

HALMASHAURI YA MANISPAA YA TEMEKE



MKATABA WA KAZI

KATI YA

**HALMASHAURI YA MANISPAA YA TEMEKE
S. L. P 46343, DAR ES SALAAM
(“MWAJIRI”)**

NA

**NDG. JUMBE MOSHI SINGILIMO
S.L.P 24401 DAR ES SALAAM
(“FUNDI”)
KWA AJILI YA**

**UJENZI WA SOKO LA TAZARA
KATIKA KATA YA TEMEKE
MANISPAA YA TEMEKE**

LGA/016/W/2021-2022/86/HQ/01

**MKURUGENZI WA MANISPAA,
HALMASHAURI YA MANISPAA YA TEMEKE
SIMU: +255222851054
NAKISHI: +255222850640
DAR ES SALAAM**

SEHEMU YA I-FOMU YA MKATABA

FOMU YA MKATABA

Mkataba huu umesainiwa leo tarehe... Mwezi 06, 2022 BAINA YA HALMASHAURI YA MANISPAA YA TEMEKE - (Hapa ataitwa "Mwajiri") kwa upande mmoja na JUMBE MOSHI SINGILIMO (Hapa ataitwa "FUNDI") kwa upande mwingine.

Kwa kuwa Mwajiri anataka kazi zifanyike yaani: **UJENZI WA SOKO LA TAZARA** kwa bei ya Mkataba wa shilingi za Tanzania Milioni ishirini na saba tu. (Tsh.27,000,000/=) Bila VAT kwa barua ya kukubali yenye **Kumb. Na. LGA/016/W/2021-2022/HQ/86/01** ya tarehe 09/06/2022 Ilikubali Nukuu ya Bei ya Fundi kwa utekelezaji na ukamilishaji wa kazi hiyo.

SASA MKATABA HUU UMESHUHUDIWA KAMA IFUATAVYO:

1. Katika Mkataba huu maneno na maelezo yatakuwa na maana sawa kama yalivyopewa katika Masharti ya Mkataba unaorejelewa na:
2. Nyaraka zifuatazo zitachukuliwa kwa pamoja na zisomeke na kutafsiriwa kuwa ni sehemu ya Mkataba huu, yaani:
 1. Fomu ya Mkataba;
 2. Barua ya Kukubali Nukuu ya Bei;
 3. Fomu ya Kuwasilisha Nukuu ya Bei;
 4. Masharti Maalumu ya Mkataba;
 5. Masharti ya Jumla ya Mkataba;
 6. Michoro;
 7. Mchanganuo wa Makadirio ya Kazi;
 8. Nyaraka nyingine zozote zinazounda sehemu ya mkataba (Kumbukumbu za ufafanuzi, tamko dhidi ya rushwa).
3. Nyaraka zote zilizotajwa hapo juu zitarejelewa hapo kama 'Mkataba' na zitachukuliwa kuwa zinakamilishana na zinajieleza sawa lakini ukitokea utata au uhitilafiano zitakuwa na umuhimu katika mfuatano wake kama zinavyoonyeshwa hapo juu.
4. Katika kuzingatia malipo yanayofanywa na Mwajiri kwa Fundi kama baadaye inavyotajwa, Fundi hapa anakubaliana na Mwajiri kutekeleza na kukamilisha kazi kwa kufuata makubaliano, kwa hali zote kulingana na vifungu vya mkataba. Mwajiri hapa anakubali kumlipa Fundi kwa kuzingatia utekelezaji na ukamilishaji wa kazi, jumla ya fedha za Tanzania kwa bei ya shilingi Milioni Ishirini na saba tu. (Tsh.27,000,000/=) Bila VAT na baadaye imerejelewa kama Bei ya Mkataba kwa nyakati na namna iliyoelezwa katika mkataba.

KATIKA KUSHUHUDIA, pande hizi zimekubaliana na kutia sahihi na muhuri katika siku na mwaka kama ulivyoandikwa hapo juu.

SEHEMUYA II -BARUA YA UKUBALI

HALMASHAURI YA MANISPAA YA TEMEKE

(Barua zote zipelekwe kwa Mkurugenzi wa Manispaa ya Temeke)

Tel: +255 22-2928132
Fax: +255 22-2928137
Barua pepe: temekemc@temeke.go.tz
Tovuti: <http://www.temeke.go.tz>



Ofisi ya Mkurugenzi,
92 Barabara ya Mandela/Taita
S.L.P 46343,
15883 -DAR ES SALAAM.

Kumb. Na. TMC/PMU/P/VOL.11/01

09/06/2022

LGA/016/W/2021 – 2022/HQ/86/01

M/S JUMBE M. SINGILIMO,

S.L.P

DAR ES SALAAM.

YAH: BARUA YA KUKUBALI NUKUU YA BEI

Hii ni kukuarifu kuwa Nukuu ya Bei yako ya tarehe 07/06/2022 ya kufanya kazi ya **Ujenzi soko la Tazara lililoathiriwa na moto** kwa bei ya Mkataba wa Shilingi za Tanzania **Milioni ishirini na saba tu (27,000,000.00)** Bila VAT kama tulivyofanya majadiliano kulingana na maelekezo ya mwaliko wa kotesheni imekubaliwa.

Unatakiwa kuweka sahihi Mkataba katika Ofisi ya Ununuzi na ugavi tarehe/06/2022 saa 4:00 Asubuhi na uanze kazi siku moja baada ya Mkataba kusainiwa.

Sahihi idhinishwa.....

Jina na Cheo cha Mweka Sahihi: KAIMU MKURUGENZI
MANISPAA YA TEMEKE

For: Municipal Director
Temeke

Jina la Mwajiri: HALMASHAURI YA MANISPAA YA TEMEKE

<p>KWA NIABA YA MWAJIRI HALMASHAURI YA MANISPAA YA TEMEKE S. L. P 46343, DAR ESSALAAM</p>	<p>SHAHIDI HALMASHAURI YA MANISPAA YA TEMEKE S. L. P 46343, DAR ES SALAAM</p>
<p>Sahihi:  TEMEKE Jina: ELIHURUMA MABELYA Tarehe: 10/06/2022 Anwani: S. L. P 46343, DAR ES SAALAM. Kazi: MKURUGENZI WA MANISPAA, MANISPAA YA TEMEKE</p> <p>Muhuri:</p>	<p>Sahihi:  MSTAKIKI MEYA MANISPAA YA TEMEKE Jina: ABDALLAH MTINIKA Tarehe: 10/06/2022 Anwani: S. L. P 46343, DAR ES SALAAM. Kazi: MEYA MANISPAA YA TEMEKE, MANISPAA YA TEMEKE</p> <p>Muhuri:</p>
<p>FUNDI MKAZI:</p>	<p>SHAHIDI WA FUNDI</p>
<p>Sahihi:  Jina: J. MOSE MOSHI SINGILIMBO Tarehe: 10/06/2022 Anwani: P.O. BOX 1404 Kazi: FUNDI MKAZI</p>	<p>Sahihi:  Jina: WAJIRA MOSHI SINGILIMO Tarehe: 10/06/2022 Anwani: P.O. BOX 1404 Kazi: FUNDI</p>